LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

LHRC

KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

KIJARIDA KUHUSU

# KUTENGANA NA KUACHANA

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*




## Unaweza kutoa taarifa za ukiukwaji wa haki kupitia

# #HakiKiganjani

SMS **0699695486**

Pakua AnroidApp
ya **Haki Kiganjani**

hakikiganjani.humanrights.or.tz

***Usipotezee, toa taarifa sasa!***

KIJARIDA KUHUSU

# KUTENGANA NA KUACHANA

**Kimeandaliwa na:**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

# YALIYOMO


1. **Maana ya Kutengana ........................................................................10**

2. **Maana ya Kuachana/Talaka ...............................................................10**

    2.1.Matokeo ya Kuachana/Talaka.............................................................................10

    2.2.Mambo ya Kuangalia kabla ya Kutoa Talaka.......................................................... 11

    2.3.Jinsi ya Kupeleka Shauri la Kuvunja Ndoa au Kutengana Mahakamani..........................................................................................................13

3. **HITIMISHO ..............................................................................................16**

## SHUKRANI

Tunatoa shukrani kwa wanasheria wetu na wale wa kujitolea katika uandaaji wa vijarida hivi. Pia tunawashukuru kwa dhati wale wote walioshiriki kwenye kukirejea kijitabu hiki ili kuandaa toleo hili la nne hususan, Wakili Joanitha Mutayoba, Wakili Theresia Kinabo, Bi. Irene Nambuo na Bwana Rodrick Maro, pamoja na wafanyakazi wote wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

## UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika binafsi la kujitolea na la hiari ambalo si la kisiaa wala kibiashara. Kituo kimeandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania mnamo mwezi Septemba, mwaka 1995. Kabla ya kusajiliwa kama chombo huru, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikuwa ni mradi wa haki za binadamu wa Mfuko wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania (TANLET). Makao makuu ya Kituo ni Dar es Salaam na Arusha kuna ofisi ndogo.

## MAONO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina taamali jamii yenye haki na usawa.

## TAMKO LA LENGO MAHUSUSI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali wala kibiashara linalojibidisha kukuza uweo wa jamii ili iweze kukuza, kuendeleza na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

## LENGO KUU

Lengo kuu la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kukuza uelewa wa sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla na hasa wale wanajamii ambao kwa sababu moja au nyingine wameachwa nyuma. Uelewa unakuzwa kwa njia ya elimu ya uraia na msaada wa kisheria.

## DIBAJI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina azma ya kusaidia jamii ya Watanzania kuwa na uwezo wa kufahamu sheria za nchi pamoja na kufahamu haki zao ili kuzilinda na kuzitetea pamoja na kuheshimu haki za wengine ili hatimaye tuwe na jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu pamoja na nchi inayoheshimu utawala wa sheria.

Tunafahamu kuwa kwa raia wa kawaida si rahisi kuzifahamu sheria zetu zote, na hata baadhi tu ya sheria zinazomgusa kutokana na mfumo tulio nao, ambao hautoi nafasi kwa watu wote kujua sheria. Hali hii inasababisha watu wengi kujikuta katika matatizo ya kisheria ambayo yangeweza kuepukika kama wangejua sheria. Ndiyo maana basi Kituo kimeamua kutoa chapisho hili na mengine, kwa lengola kutoa msaada wa kisheria kwa raia.

Huu ni usaidizi kisheria unaotoa maelezo mafupi na ya msingi ya kisheria ili kukusaidia ndugu msomaji uweze kupata ufumbuzi au maelezo ya tatizo linalokusibu. Ni lengo letu kuwa, katika kijitabu hiki tunatoa usaidizi wa moja kwa moja kwako wewe pale utakapokuwa na tatizo

au mmoja wa ndugu au jamaa zako wanapopata matatizo ya kisheria.
Tunachokuomba ni wewe kusoma kwa makini; na pale suala lako linapokwenda mbali zaidi ya maelezo haya, basi utafute msaada wa kisheria au uende kwa mwanasheria aliye karibu na wewe ili aweze kukusaidia.

Tunaamini utapata usaidizi huu kiurahisi zaidi na maelezo yaliyomo humu yatakusaidia kwa karibu. Umalizapo, tafadhali mshirikishe na mwingine ili aweze kunufaika na elimu hii.
Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

# UTANGULIZI

Kwa kawaida watu wawili waliooana wanaweza kufikia hatua ya kutoelewana. Hatua hii ikiendelea wanandoa hao hushauriwa kutengana au kuachana. Hii huashiria kuvunjika kwa mkataba wa ndoa. Kwa hiyo basi mkataba huu unapofikia hatima na kuvunjika ni mahakama peke yake ndiyo yenye mamlaka ya kutamka kuwa ndoa imevunjika kiasi kwamba haiwezi kurekebishika tena na kutoa amri ya kuvunja ndoa husika. Hata hivyo wengine hupendelea kutengana kwanza kwa makubaliano yao wenyewe au kwa maelekezo ya mahakama ili kutoa nafasi ya kurudiana pindi uhusiano wao wa kimapenzi utakaporejea. Katika hali hii, mahakama zinaweza kuwatenganisha kwa mujibu wa sheria. Sheria inayotawala masuala ya kuachana na kutengana ni sheria ya Ndoa ya mwaka 1971.

# 1. MAANA YA KUTENGANA

Kutengana ni kitendo cha wanandoa (Mume na Mke) kwa amri ya mahakama au hiari yao wenyewe kuishi mbali mbali kwa muda. Kutengana kwa wanandoa hutokana na wanandoa hao kutoelewana. Mume au Mke ana haki ya kuomba mahakama kutoa amri kutenganishwa na mwenza wake. Baada ya muda fulani wanandoa hao wanaweza kurudiana tena au kuachana kabisa.

# 2. MAANA YA KUACHANA/TALAKA

Talaka ni amri inayotolewa na mahakama kuwaamuru wanandoa kuachana milele pale inapodhibitika kuwa ndoa hiyo haiwezi kurekebishika tena Mume au mke anaweza kuiomba mahakama itoe talaka.

### 2.1. Matokeo ya Kuachana/Talaka

- » Ndoa kuvunjika;
- » Mgawanyo wa mali zilizochumwa kwa pamoja na wanandoa; na
- » Matunzo na malezi ya watoto kama wapo.

**MUHIMU:**

Kwa kawaida hairuhusiwi kuvunja/kutengana au kuomba talaka mahakani kabla ya muda wa miaka miwili kupita tangu wanandoa hao waoane isipokuwa kwa ruhusa/hati ya mahakama, na hati hiyo ya mahakama itatolewa ikiwa itathibitika kuwa mwombaji ana hali ngumu isiyo ya kawaida, isiyoweza kuvumilika kwa muda huo wa miaka miwili.

## 2.2. Mambo ya Kuangalia kabla ya Kutoa Talaka

Kwa kawaida mahakama hutoa talaka inapothibitisha kwamba ndoa hiyo imevunjika kiasi cha kutokurekebishika tena. Mahakama itathibitisha kwamba ndoa hii imevunjika kiasi cha kutokurekebishika kwa kuangalia mambo au vigezo vifuatavyo:-

a. Ikiwa mmoja wa wanandoa hao atathibitika kufanya uzinzi (ugoni);

b. Ikiwa mmoja wa wanandoa hao alithibitika kumfanyia ukatili wa kimwili au kiakili mwanandoa mwenzake au watoto wao;

c. Iwapo itathibitika kuwa mmoja wa wanandoa hao amemtelekeza mwenzake na kwenda kuishi mbali au kumtekeleza akiwa ndani ya nyumba (kwa kuhama chumba, kitanda au kuishi nyumba ya pili kati ya wanazomiliki bila ridhaa /idhini ya mwenzake);
d. Uasi au utoro;
e. Kutelekeza familia kwa makusudi kwa muda usiopungua miaka mitatu (3);
f. Kutengana kwa hiari au kwa amri ya mahakama kwa kipindi kisichopungua miaka 3;
g. Kifungo gerezani kisichopungua miaka mitano (5) au kifungo cha maisha;
h. (Kichaa kisichotibika ambacho kimethibitishwa na madaktari bingwa wa akili wasiopungua wawili (2);
i. Tofauti ya itikadi za kidini au siasa.

### 2.3. Jinsi ya Kupeleka Shauri la Kuvunja Ndoa au Kutengana Mahakamani

Kabla shauri hilo halijapelekwa mahakamani, ni lazima lipitie kwenye baraza la usuluhishi la ndoa linalotambulika kisheria. Mwanandoa anayetaka kufanya hivyo anaweza kupeleka shauri hilo katika baraza la usuluhishi la ndoa ambalo linaweza kuwa la kidini au baraza la usuluhishi la ndoa la kata. Baraza linatakiwa kuwasikiliza na kuwasuluhisha wanandoa, endapo baraza litashindwa kuwasuluhisha, litatoa taarifa/ hati itakayowasilishwa mahakamani juu ya kushindwa huko ili Mahakama iendelee kuamua itakavyoona inafaa.

Hata hivyo, sharti la kupeleka shauri la ndoa kwenye baraza la usuluhishi laweze kuepukwa endapo tu itathibitika kuwa zipo sababu za msigi za kufanya hivyo.

Sababu hizo zinaweza kuwa:-

a. Mwanandoa mmoja kumtelekeza mwenzake na hajulikani alipo kwa muda mrefu.

b. Iwapo mwanandoa mmoja anaishi nje ya nchi.
c. Ikiwa mwanandoa mmoja amefungwa kifungo cha maisha au kuhukumiwa kunyongwa.
d. Ikiwa mwanandoa mmoja anaugua ugonjwa wa akili usiopona.
e. Ikiwa mahakama itaridhika kuwa zoezi la kupeleka shauri Baraza la usuluhishi la ndoa halitazaa matunda yeyote.
f. Ikiwa itaonekana kuwa mmoja wa wanandoa hao ni mgomvi n.k

Baada ya usuluhishi kushindikana na baraza la usuluhishi la ndoa kutoa hati kwa upande unaotaka kupeleka shauri mahakamani mhusika ataandaa hati ya kuomba kuvunja ndoa au kutenganishwa kwa muda, itakayo ambatanishwa na hati ya baraza la usuluhishi na kupelekwa mahakamani.

Mwanandoa ambaye anadai kutengana au kuachana atafungua shauri la ndoa Mahakamani akidai moja au zaidi ya mambo yafuatayo:-

i. Kutengana
ii. Kuachana
iii. Mgawanyo wa mali
iv. Uangalizi wa watoto
v. Matunzo ya watoto
vi. Matunzo kwa mwanandoa ambaye hana uwezo wa kujikimu.

Ikumbukwe kuwa kipindi chote ambacho wanandoa watakuwa wametengana au kuachana baba ana wajibu wa kuendelea kuhudumia familia.

# 3. HITIMISHO

Msomaji wetu, ni matumaini yetu kwamba mpaka sasa unajua ni nini tofauti ya kutengana au kupeana talaka. Kutengana huwa inakuwa ni kwa muda fulani tu na inaweza kuwa ni kwa amri ya mahakama au ridhaa ya wanandoa.

Wakati kuachana/kupeana talaka ni amri ya mahakama pekee na amri hii ni ya moja kwa moja siyo ya muda. Ila katika kuachana kuna mambo yatatakiwa kufanyika kutokana na mahakama itakavyoamua. Pia tumeona kuwa ni lazima shauri lipitie baraza la usuluhishi kabla ya kupelekwa mahakamani. Ni muhimu kuzingatia hili kwani hati ya kuomba kuvunja ndoa haitasilkilizwa bila kuambatanishwa na hati ya baraza la usuluhishi, labda tu kutokana na mazingira yaliyoainishwa hapo juu ambapo hati ya baraza sio muhimu.

**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU**
S. L. P. 75254, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu:** +255 22 2773038/48  **Nukushi:** +255 22 2773037
**Barua Pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

**DODOMA OFFICE**
Kitalu na 22. Area D,
S.L.P  2289, Dodoma, Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 262350050
**Barua pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

**Ofisi ya Arusha**
Barabara ya Olerian, Olosiva Kitalu Na. 116/5,
Sakina kwa Idd, Arumeru
S. L. P. 15243, Arusha - Tanzania
**Simu:** +255 27 2544187
**Barua Pepe:** lhrcarusha@humanrights.or.tz

**Kituo cha Msaada wa Sheria**
Mtaa wa Isere - Kinondoni
S. L. P. 79633, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 22 2761205/6
**Barua Pepe:** legalaid@humanrights.or.tz

@humanrightstz    HakiTV

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*